# TANZANIA TUNAYOPIGANIA

## ILANI YA UCHAGUZI MKUU

## 2015

ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 1 8/27/15 3:32 PM

ACT Wazalendo

@ACTwazalendo

**www.act.or.tz**
**www.actwazalendo.or.tz**

House N°203, Mpakani A Street, Kijitonyama, P.O. Box 105043, Dar es salaam/ Tel: +255 763 463740 / 715 784670



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 2 8/27/15 3:32 PM

# 1. UTANGULIZI: ITIKADI, FALSAFA NA IMANI YA ACT WAZALENDO

1.1 ACT Wazalendo inaamini katika misingi ya Ujamaa wa kiDemokrasia (Democratic Socialism) ikiwa na ngao nne zifuatazo:

i) Udugu ni hifadhi ya jamii ya asili kwa Waafrika, na hivyo kila mtanzania na kila mwafrika ana jukumu la kumsaidia mwenzake anayekabiliwa na tatizo au janga popote alipo bila kutarajia malipo ya aina yoyote.

ii) Serikali kusimamia maendeleo ya nchi kwa kuwa na haki na wajibu wa kuendesha moja kwa moja sekta nyeti katika jamii zenye maslahi mapana ya kiusalama na kiuchumi kwa nchi bila kuathiri nafasi ya sekta binafsi kuendesha shughuli za uzalishaji mali na utoaji wa huduma;

iii) Viongozi na watumishi wa umma wana wajibu wa kuhakikisha kwamba wanaishi na kuenenda katika misingi inayolinda heshima ya ofisi za umma na kwamba hawatumii nafasi zao kwa manufaa yao binafsi na jamaa zao. Ili kuwasaidia na kuwawezesha viongozi na watumishi wa umma kuenenda katika misingi ya uadilifu, Miiko ya Viongozi itakuwa ni kanuni ya lazima kufuatwa na kila mtu wenye dhamana ya umma.



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 1 8/27/15 3:32 PM

iv) Demokrasia ndiyo msingi wa maendeleo ya kijamii, kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa na kwamba demokrasia ndiyo msingi wa ujenzi wa taifa huru na linaloheshimu na kuzingatia utawala wa sheria.

1.2 ACT Wazalendo inatambua kuwa sisi wananchi wa Tanzania ndiyo raslimali kubwa ya nchi, na kwamba nchi yetu imejaliwa rasilimali nyingi ambazo zikivunwa na kutumika vizuri zinaweza kuboresha maisha na kuchangia katika maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla. Hivyo basi, shabaha kuu ya ACT Wazalendo ni kuhakikisha kuwa utajiri wa nchi unatumika kuboresha maisha ya watu na kuchochea uwezo wao katika kuchangia kujenga uchumi shirikishi ambapo kila mtu ana fursa sawa za maendeleo.

1.3 Falsafa ya ACT Tanzania ni UNYERERE, ikiwa ni dhamira ya kurudisha, kuhuisha na kupigania misingi mama iliyoasisi Taifa la Tanzania, kama ilivyoanishwa katika Azimio la Arusha ambalo lilipitishwa na Halmashauri Kuu ya TANU mwaka 1967 na kama lilivyohuishwa na Chama cha ACT Wazalendo kwa mazingira ya Tanzania ya sasa, pamoja na shabaha ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964, ikiwa na imani kwamba:

i) Binadamu wote ni sawa;

ii) Kila mtu anastahili heshima;

iii) Kila raia ana uhuru kamili wa kutoa mawazo



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 2 8/27/15 3:32 PM

yake, kwenda anakotaka na kuamini dini anayotaka na kukutana na watu wengine bila kuvunja sheria;

iv) Kila mtu ana haki ya kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake na mali yake aliyo nayo kwa mujibu wa sheria;

v) Kila mtu anayo haki ya kupata malipo ya haki kutokana na kazi yake;

vi) Raia wote kwa pamoja wanamiliki utajiri wa asili wa nchi hii ukiwa kama dhamana kwa vizazi vyao;

vii) Serikali ina mamlaka na wajibu wa kusimamia njia muhimu za kukuza uchumi.

# 2. MISINGI YA ACT WAZALENDO

ACT Tanzania inaongozwa na Misingi Kumi (10) ifuatayo:

## i) Uzalendo

Ili wananchi waweze kushiriki katika utumishi wa umma na kutoa michango yao mbalimbali kwa dhati na kwa moyo, ni muhimu mazingira yawepo ya kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa na mapenzi yasiyotikisika kwa nchi yao. Kwa msingi huu, ACT Wazalendo itajenga mazingira mwafaka ya wananchi kuipenda nchi yao ili wajitoe kikamilifu katika kuijenga na kuilinda.

## ii) Usawa

ACT Wazalendo inaamini katika usawa katika nyanja zote. Tunaamini kwamba mafanikio ya mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla yatatokana na bidii katika kazi. Kwahiyo, ACT Wazalendo kitapigania kuwepo usawa wa fursa na mazingira mazuri kwa watu wote katika kuhakikisha kwamba kila mtu na kila kundi katika jamii linakuwa na fursa sawa ya kufanya kazi za kujiajiri au kuajiriwa, na kwamba kipato kitokanacho na kazi halali ndicho kitakuwa kipimo cha mchango wake katika jamii na taifa.

## iii) Kupinga na Kupiga Vita ubaguzi

Sambasamba na msingi wa usawa, ACT Wazalendo inapinga na kupiga vita aina zote za ubaguzi. Hivyo basi chama na serikali itokanayo itahakikisha inatoa fursa sawa kwa watu wote bila kujali tofauti zao za kinasaba

## iv) Uadilifu

Uadilifu katika maisha binafsi na katika jamii utakuwa ndio msingi na mwongozo mkuu wa viongozi na wanachama wa ACT Wazalendo. ACT Wazalendo inaamini kwamba uadilifu ndio msingi na nguzo kuu ya mapambano dhidi ya rushwa na maovu mengine katika jamii. Kama wanachama wa ACT Wazalendo tutajitahidi wakati wote kutumikia na kuishi kwa uadilifu uliotukuka siyo tu kama taasisi bali pia katika maisha yetu binafsi.



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 4 8/27/15 3:32 PM

### v) Uwazi

ACT Wazalendo inaamini katika uwazi kwenye mambo yote ya kijamii na kitaifa. Hivyo basi viongozi na wanachama wa ACT Wazalendo wana wajibu wa kupigania uwazi katika mambo yote wanayofanya kwa ajili ya umma. Uwazi huu ni msingi wa kupambana na vitendo vya ukosefu wa maadili na ufisadi na hivyo tunaamini njia sahihi ni kuhakikisha kuwa wanachama na wananchi waliotupa dhamana ya uongozi wanajua yanayofanywa na chama na serikali yao.

### vi) Uwajibikaji

Sambamba na uwazi, ACT Wazalendo inaamini kwamba kila mwananchi na kiongozi mwenye dhamana katika umma ana wajibu katika jamii na Taifa kwa ujumla na ni jukumu lake kutekeleza wajibu huo bila kinyongo. Aidha, mwanachama na kiongozi atokanaye na ACT Wazalendo anapaswa kuwajibika kwa maneno na matendo yake katika utumishi au nje ya utumishi wa chama au taasisi yeyote ya umma.

### vii) Demokrasia

ACT Wazalendo inaamini kuwa demokrasia ndiyo msingi wa kujenga fikra pevu na kueneza uhuru wa mtu, jamii na Taifa kwa ujumla. Hivyo basi, viongozi na wanachama wa ACT Wazalendo watapigania uwepo wa demokrasia ya kweli katika kila ngazi, ndani na nje ya chama.



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 5 8/27/15 3:32 PM

### viii) Uhuru wa Mawazo na Matendo

ACT Wazalendo inaamini kuwa uhuru wa mawazo na matendo ni asili ya binadamu. Hivyo basi chama na serikali itokanayo itaweka mazingira kuhakikisha kwamba uhuru wa mawazo na matendo wa wanachama na wananchi kwa ujumla unalindwa.

### ix) Utu

ACT Wazalendo inaamini kuwa sera, mipango na shughuli zozote za kichama au za kiserikali zitakuwa hazina mafanikio ya kudumu kama hazitatambua, kuheshimu na kulinda utu wa kila Mtanzania. Ni kwa sababu hiyo tunu kuu itakayotuongoza katika utumishi wa umma ni kuheshimu, kutambua na kulinda utu wa kila mtu bila kujali tofauti zozote ambazo zinawatofautisha watu.

### x) Umoja

Chama cha ACT Wazalendo kinaamini katika umoja wa bara la Afrika na itikadi ya umajumui wa Afrika. Sera za chama zitajengwa katika kuelekeza nchi yetu inachukua uongozi katika kujenga Shirikisho la Afrika Mashariki kama msingi wa kujenga Afrika moja imara na yenye sauti kwenye mataifa ya ulimwengu.



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 6 8/27/15 3:32 PM

# 3. TANZANIA TUNAYOIPIGANIA

Tanzania ni zaidi ya mkusanyiko wa watu na vitu vilivyomo. Msingi wa ujenzi wa Taifa ulikuwa ni UZALENDO uliochochewa na itikadi, falsafa na imani imara. Hata hivyo, katika siku za karibuni utaifa wa Taifa la Tanzania umetikiswa. Nchi sasa imeanza kugeuka kuwa mkusanyiko tu wa watu wanaohangaika kutafuta vitu na ambao wanatumia muda mwingi kuimarisha 'vitaifa' vyao kupitia vyama vyao vya siasa, dini zao na hata kabila zao.

Kuna haja ya kufufua uzalendo, upendo, umoja na mshikamano wa watanzania wote bila kujali rangi, kabila, dini, jinsia na wala ufuasi wa chama cha siasa.ACT Wazalendo tunataka kufufua utaifa wa Tanzania ili kila Mtanzania aone kuwa ana wajibu wa kujenga nchi yake kwa ajili ya leo na vizazi vijavyo.

Serikali itakayoundwa na ACT Wazalendo itaweka vipaumbele vitakavyochochea uwajibikaji na tija ya haraka kwa kila mtanzania, na kuhakikisha kwamba uchumi unaendelea kukua kwa kasi na kiwango ambacho kila mtanzania anaona matunda ya kukua kwa uchumi huo.

## Ndoto

Taifa lenye kujitegemea kiuchumi na kiutamaduni, na ambalo linalinda na kudumisha usawa, ustawi wa jamii, uwajibikaji, demokrasia na uongozi bora.



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 7 8/27/15 3:32 PM

## 4. HAIBA NA TASWIRA YA SERIKALI YA ACT WAZALENDO

Haiba na taswira ya serikali ya ACT Wazalendo itaonekana katika maeneo manne yafuatayo:

i) Serikali inayowajibika na kuwaheshimu wananchi kupitia matokeo ya kazi zake: Katika kutekeleza hili:

   a. Kila wizara itakuwa na mpango kazi wenye malengo mahsusi na utakaowekwa wazi kwa umma. Utendaji na ufanisi wa kila wizara utapimwa kwa kuzingatia mpango huo wa kazi.

   b. Bajeti ya serikali na wizara zote itapangwa kwa kuzingatia mpango kazi wenye malengo mahsusi na viashiria vya matokeo vinavyopimika.

ii) Serikali inayoheshimika kwa kuundwa na viongozi wazalendo, weledi na wachapa kazi na ambao hawana mawaa katika jamii na ambao watarudisha heshima ya Tanzania katika ramani ya ulimwengu na kufanya wananchi waipende na kuitumikia nchi yao kwa moyo na bidii.

iii) Serikali inayochukizwa na kupambana na wala rushwa kwa vitendo. Ili kutekeleza hili tutahakikisha kwamba:

   a. Kila mtu anatii na kuzingatia utawala wa sheria.

   b. Watumishi wa umma wanaajiriwa kwa mujibu wa sifa za weledi na bidii katika kazi na wanapata mafunzo stahiki kwa ajili ya kuimarisha utendaji wao.



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 8 8/27/15 3:32 PM

c. Hatua za kisheria na kinidhamu zinachukuliwa haraka kwa wale wote wanaopatikana na vitendo vya kula rushwa.

d. Kila kiongozi wa umma na wa chama atafuata kanuni maalumu za maadili kwa kuweka wazi maslahi yao kupitia tangazo la mali na madeni ambalo litawekwa wazi kwa wananchi wote kuona, kuhoji na mfumo wa malalamiko juu ya usahihi wa tamko.

iv) Serikali ya uwazi na inayowajibika kwa wananchi. Serikali itahakikisha kwamba kila uamuzi unaochukuliwa na serikali unajulikana kwa wananchi. Utii wa serikali ya ACT Wazalendo itakuwa kwa wananchi. Kila uamuzi utakaochukuliwa utapimwa kwa kigezo cha 'Uamuzi huu una maslahi gani kwa wananchi na nchi sasa na baadaye'.

**Kauli mbiu ya ACT Wazalendo katika uchaguzi wa mwaka 2015 itakuwa ni Utu, Uzalendo na Uadilifu.**

Kauli mbiu hii inaakisi hali ya nchi yetu hivi sasa kwamba kuna haja ya kujenga utu ili kila mtanzania aheshimiwe na kuthaminiwa, kujenga uzalendo ili Watanzania waipende nchi yao na wajivunie nayo na kusimika uadilifu kwa kujenga mfumo madhubuti wa uwajibikaji ili kupambana na rushwa na ufisadi.

# 5. VIPAUMBELE VYA SERIKALI YA ACT WAZALENDO

Serikali ya ACT Wazalendo itawajibika kwa wananchi na Taifa kwa kuwekeza katika maeneo manne ya kipaumbele yafuatayo:

i) Hifadhi ya jamii

ii) Uchumi shirikishi wenye kuzalisha Ajira nyingi na bora

iii) Afya

iv) Elimu

## 5.1 Hifadhi ya Jamii

Hifadhi ya jamii ni mfumo imara na endelevu wa kuwajengea uwezo na utayari wananchi katika kukabiliana na matatizo na majanga ya kiuchumi na kijamii. Hifadhi ya jamii husaidia sana kutoa usalama na uhakika wa kiuchumi, kijamii na kiafya. Hii ni njia ambayo serikali, mwajiri na mwajiriwa huchangia kiasi fulani cha mapato yake ya sasa kwa ajili ya kumsaidia baadaye atakapokuwa hana uwezo wa kupata kipato cha uhakika. Aidha, hifadhi ya jamii husaidia wafanyakazi katika sekta ya umma na binafsi kukabiliana na gharama matibabu na matatizo mengine ya kijamii.

Tafiti zinaonyesha kuwa uwepo wa hifadhi ya jamii kwa watu wengi iwezekanavyo katika nchi



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 10 8/27/15 3:32 PM

huchangia kupunguza hali ya umaskini na hivyo kuipandisha nchi kiuchumi na kijamii. Hifadhi ya Jamii pia huchochea uwekaji akiba katika nchi na hivyo kuwezesha uwekezaji wa ndani na kupanua shughuli za uzalishaji mali.

Hapa Tanzania hifadhi ya jamii hupatikana kwa wananchi waliojiriwa pekee katika sekta ya umma na binafsi. Kwa sababu hii ni asilimia 6 tu ya nguvu kazi ya Watanzania ndiyo waliopo katika mfumo rasmi wa hifadhi ya jamii. Ndiyo kusema, watu wengi nchini hawana namna rasmi ya kujiandaa na namna ya kuishi baada ya kuishiwa nguvu za kufanya kazi kwa sababu ya uzee, magonjwa au ulemavu. Hii inachochea umaskini kwa sababu kundi kubwa la watu wanaostaafu hujikuta hawana namna ya kuishi na hivyo kutumbukia katika wimbi la umaskini.

Aidha, kukosekana kwa mfumo rasmi wa hifadhi ya jamii umefanya watu wengi wasiwe na uwezo na mfumo mzuri wa matibabu. Vile vile kukosekana kwa mfumo imara wa Hifadhi ya Jamii kumesababisha uwekaji akiba nchini kuwa hafifu ( 16% tu ya Pato la Taifa ). Kwa Uchumi kama wa Tanzania unaokua kwa wastani wa 7%, ili kuondoa umasikini inahitajika uwekaji akiba wa 35% ya Pato la Taifa na zaidi. Nchi ya China inayokua kwa 10% uwekaji akiba wake ni 50% ya Pato la Taifa.

Ili kuwezesha wananchi wengi zaidi kuingia katika mfumo wa hifadhi ya jamii, Serikali ya



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 11 8/27/15 3:32 PM

ACT Wazalendo itachukua hatua zifuatazo:

1) Kutumia Hifadhi ya Jamii kama nyenzo *(instrument)* ya kukuza uwekaji akiba nchini ili kuwa na vyanzo vya mitaji ya uwekezaji wa ndani.

2) Kupanua hifadhi ya jamii na kufikia wakulima, wafugaji na wananchi wengine waliojiajiri kwa kutunga sheria itakayopelekea Serikali kuchangia theluthi moja ya kila mchango wa mwananchi atakayechangia kima cha chini cha michango kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

3) Kutumia Hifadhi ya Jamii kuwezesha wananchi kujiwekea akiba kupitia vyama vyao vya ushirika kama SACCOS na kupata mikopo ya gharama nafuu ili kuanzisha biashara ndogondogo, kupata Bima ya Afya na kuhimili mahitaji kama ya kusomesha watoto wao.

4) Kutumia Hifadhi ya Jamii kuwekeza kwenye miradi mikubwa kama miundombinu ya kilimo, viwanda vya kusindika mazao ya kilimo, vyuo vya ufundi na miundombinu kama reli kwani kwa uasili wake madai dhidi ya mifuko *(liabilities)* ni ya muda mrefu.

5) Kuanzisha mfumo ambao kila Mtanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 60 na kuendelea kupata pensheni.

6) Kutunga Sheria kuwezesha mifuko ya Hifadhi ya Jamii kutoa mafao ya Bima ya Afya, Bima za Mazao na majanga *(Crop Insurance)* kwa kilimo na mifugo na Fao la Bei *(Price Stabilization Benefit)*.

7) Kuboresha sheria ya Hifadhi ya Jamii kwa kuunganisha Mifuko iliyopo sasa na kubakia na mifuko 3 tu; Mfuko wa Bima ya Afya, Mfuko wa Sekta ya Umma *( Public Sector Pension Scheme)* na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(National Social Security Scheme)* ambao utahusisha sekta binafsi na sekta isiyo rasmi *(informal sector)*.

8) Kuimarisha Utawala bora wa Mifuko kwa kuweka masharti ya uwazi *(disclosure rules)* katika uwekezaji wa mifuko ili kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za Mifuko na kuwa na miradi yenye tija kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

9) Kuweka mfumo thabiti wa kuhakikisha wajibu wa Serikali katika kuhudumia watoto yatima na wananchi wanaoishi katika mazingira magumu.

10) Kuhamasisha wananchi wajielimishe kuhusu umuhimu na namna ya kushiriki katika hifadhi ya jamii

Hatua hizi katika Hifadhi ya Jamii zitapelekea kuwepo kwa akiba ya tshs 1.8 trilioni kila mwaka kwa ajili ya uwekezaji wa ndani kwa makisio kuwa

Watanzania milioni tano tu watakuwa kwenye Hifadhi ya Jamii na kuchangia kima cha chini kabisa kwa mwezi. Hii ni sawa na 2.5% ya Pato la Taifa na hivyo kuwezesha uwekezaji mkubwa kwenye Kilimo na Viwanda vya kuongeza bidhaa za kilimo, pia uwekezaji mkubwa kwenye Elimu kwa kujenga vyuo vya Ufundi Stadi kila Wilaya na katika kila kambi ya JKT na vyuo vya Ufundi mchundo kila mkoa.

## 5.2 Uchumi shirikishi wenye kuzalisha Ajira nyingi na bora

Watanzania walio wengi bado wanategemea kilimo cha asili kama ajira yao. Kwa mujibu wa takwimu za Kituo cha Taifa cha Takwimu (NBS), sekta ya kilimo cha asili kinaajiri takribani robo tatu (75%) ya watanzania wote. Kwa vijijini asilimia 89 ya wananchi wanategemea kilimo wakati mijini ni asilimia 44. Kwa upande wa miji mikubwa kama vile Dar es Salaam asilimia kubwa (38%) ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi wamejiajiri wenyewe au wapo katika ajira zisizohusiana na kilimo. Fursa za ajira katika mfumo rasmi bado ni finyu sana.

Tafiti zinaonyesha kuwa tatizo la ajira nchini Tanzania na nchi zingine za kiAfrika ni ukosefu wa maarifa na stadi za kazi zinazowafanya wahitimu katika ngazi mbalimbali za elimu wasiajirike. Aidha, ufinyu wa sekta za uzalishaji na huduma unasababisha ufinyu wa nafasi za ajira. Ifikapo mwaka 2030 kutakuwa na watu



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 14 8/27/15 3:32 PM

milioni 25 zaidi katika soko la ajira, wastani wa watu 1.6 milioni kuingia katika nguvu kazi ya Taifa kila mwaka. Iwapo Taifa halitakuwa na mipango sahihi, badala ya kufaidika *(demograpic dividend)*, tutapata janga kubwa na machafuko.

Ili kukabiliana na ukosefu wa ajira nchini, Serikali ya ACT Wazalendo inalenga kutengeneza Taifa linalofanya kazi *(a working nation)* kwa kuchukua hatua zifuatazo katika sekta za Kilimo, Viwanda, Utalii na Madini, Mafuta na Gesi Asilia

### 5.2.1 Kilimo

Ili kujenga uchumi shirikishi, ni muhimu kufanya jitihada za makusudi katika kuhakikisha kwamba kilimo chetu kinaanza kuchangia vya kutosha katika ukuaji wa uchumi.

**Shabaha ya muda wa kati katika sekta ya kilimo ni kuongeza Mapato ya Fedha za kigeni kutokana na kilimo ikiwemo kilimo cha maua na mbogamboga hadi kufikia dola za kimarekani bilioni mbili kwa mwaka ifikapo mwaka 2025.**

**Shabaha ya muda mrefu ni kujitosheleza kwa chakula na ziada kuuza nje na kuongoza katika nchi za Afrika Mashariki kwa kuuza nje Sukari na Mchele; Kurejea kuwa nchi ya kwanza duniani kwa kuuza nje Katani na bidhaa za Katani; Kuongoza Afrika kwa kuuza nje Korosho zilizokobolewa na Wakulima wote wa Tanzania kuwa na hifadhi ya jamii.**



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 15 8/27/15 3:32 PM

Chama cha ACT Wazalendo kitaagiza serikali kuchukua hatua mahususi zifuatazo kuhusu kilimo:

1) Kilimo ndio shughuli kiongozi katika kutokomeza umasikini. Shughuli za Kilimo lazima ziendeshwe na wananchi wenyewe kwa kuwawezesha kumiliki ardhi, kuongeza tija na hivyo uzalishaji na kupata mitaji kwa kupitia mfumo wa hifadhi ya jamii.

2) Mfumo wa Hifadhi ya Jamii uwekewe utaratibu wa kuwepo kwa fao la Bei ya mazao *(price stabilization)*, Bima ya Mazao na Mifugo na mikopo ya gharama nafuu kwa vikundi vya wakulima ili kununua pembejeo za kilimo na ufugaji kwa lengo la kuhami mwananchi asitumbukie kwenye ufukara.

3) Ardhi na mashamba yote yaliyokuwa ya Mashirika ya Umma na kubinafsishwa yarejeshwe kwa wananchi wasio na ardhi kwa kuwagawia na kushiriki katika uzalishaji kwa kutumia mfumo wa *'outgrowers scheme'*.

4) Mashamba makubwa ya kibiashara yatakapohitajika itakuwa ni jumla ya mashamba madogo madogo ya wananchi na pale uwekezaji utakapohitaji basi wananchi watamiliki theluthi mbili ya shamba husika na mwekezaji wa ndani au wa nje atamiliki theluthi moja tu.

5) Serikali itunge mfumo wa kodi unaoeleweka na usiotetereka *(stable fiscal regime)* katika sekta ya kilimo ili kuhakikisha kuwa mkulima anabakia na sehemu kubwa ya mapato yake.

6) Serikali iunde Mamlaka ya Kilimo ili kusimamia sekta ya kilimo. Wajibu wa kuhakikisha mazao ya kilimo ya wananchi yote yamenunuliwa kwa bei nzuri utakuwa wajibu wa Serikali kupitia Shirika la Umma litakaloundwa mahususi kwa kazi hiyo.

7) Dola kuhusika kikamilifu kwenye hifadhi ya mazao na kuanzisha mfumo wa soko kupitia soko la bidhaa *(commodities exchange)* ambao utashirikisha vyama vya wakulima na hivyo kufuta kabisa watu wa kati *(middlemen)*.

8) Mfumo wa usambazaji wa pembejeo za kilimo utapaswa kurekebishwa ili kutoa nguvu kwa vyama vya msingi vya wakulima kununua pembejeo zao wenyewe kwa wakati. Serikali itakuwa na wajibu wa usambazaji wa pembejeo kwa wakulima kupitia Shirika la Umma litakalokuwa na wajibu huo pekee.

### 5.2.2 Viwanda

**Shabaha ya muda wa kati ni kuhakikisha kuwa bidhaa za viwanda zinaliingizia Taifa mapato ya fedha za kigeni zaidi ya dola za kimarekani bilioni tatu kwa mwaka.**



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 17 8/27/15 3:32 PM

Msukumo utawekwa kwenye bidhaa za nguo kwani zinaajiri watu wengi zaidi na mnyororo wake wa thamani ni mrefu mpaka kwa wakulima wa pamba nchini. Itakuwa ni marufuku kuuza nje malighafi *(raw materials)* isipokuwa kwa mazingira maalumu ikiwemo inapothibitika kuwa uwezo wa ndani wa nchi ni mdogo.

Chama cha ACT Wazalendo kitaagiza serikali kuchukua hatua mahususi zifuatazo kuhusu viwanda:

1) Viwanda, vikiwemo vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi vipewe kipaumbele kikubwa kwa kuwekewa vivutio vya kodi ikiwemo ruzuku za kufidia gharama za uzalishaji kama umeme (mfano viwanda vya kuzalisha sukari, saruji, ngozi, korosho na nyuzi za Pamba) na zawadi za kodi *(exports tax credits)* ili kuchochea mauzo ya nje.

2) Kupiga marufuku kuuza nje malighafi baada ya kipindi cha mpito kitakachowekwa.

3) Serikali ishiriki katika umiliki wa viwanda vya msingi kama vile viwanda vya chuma cha pua na kusimamia kikamilifu ushiriki wa sekta binafsi katika kuongeza uzalishaji viwandani.

4) Kujielekeza kwenye soko la Kanda kwani Viwanda vya Tanzania vina fursa ya kuuza ndani ya Afrika Mashariki, Kati na Maziwa



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 18 8/27/15 3:32 PM

Makuu bidhaa kama unga, plastiki, saruji, sukari na vinywaji maradufu ya mauzo ya sasa. Hivyo serikali ihakikishe kwamba soko la kanda linakuwa ni kipaumbele cha kwanza katika uimarishaji wa viwanda.

5) Kuweka utaratibu wa kisheria wa kufidia baadhi ya gharama za uzalishaji kwa viwanda vinavyozalisha bidhaa za matumizi muhimu ya wananchi kama Sukari na Saruji kwa lengo la kulinda ajira za Watanzania kwa kulinda viwanda vyetu.

6) Kuchochea uwekezaji kwenye viwanda vyenye kutoa ajira nyingi *(light manufacturing industries)* na viwanda vya msingi vinavyotumia maliasili tuliyonayo hapa nchini.

7) Kuchangamkia fursa ya kuhama kwa uzalishaji wa viwanda kutoka China kuja Afrika kwa kuweka mazingira bora na yenye faida kwa Taifa letu.

### 5.2.3 Utalii

**Shabaha ya muda wa kati ni Tanzania iwe na uwezo wa kuingiza na kuhudumia watalii milioni 5 kwa mwaka na kuingiza mapato ya fedha za kigeni yasiyopungua dola za kimarekani bilioni 8 kwa mwaka.** Makusudio ya Serikali katika sekta ya utalii itakuwa si kukusanya kodi tu bali ni kuzalisha ajira na kuongeza mapato ya fedha za kigeni.



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 19 8/27/15 3:32 PM

Sekta ya utalii ina nafasi kubwa sana ya kuzalisha ajira kwa vijana na wananchi kwa ujumla. Pia mnyororo wa thamani wa sekta utalii ni mrefu na kwa kuwa nchi imejaaliwa vivutio vingi vya utalii inaweza kuleta fedha nyingi za kigeni kuweza kununua mashine na vipuri tusivyoweza kuzalisha wenyewe katika kipindi cha mpito. Thamani ya fedha za kigeni katika utalii lazima ziendane na thamani ya manunuzi yetu nje ya nchi na hasa mafuta ambayo yanatumia sehemu kubwa ya akiba yetu ya fedha za kigeni.

Chama cha ACT Wazalendo kitaagiza serikali kuchukua hatua mahususi zifuatazo kuhusu utalii:

1) Kuweka mfumo rahisi wa kikodi katika sekta *(simple and stable fiscal regime)* kwa kuondoa msururu wa kodi na mamlaka za makusanyo ya kodi na tozo mbalimbali.

2) Kuweka vivutio na urahisi wa kupanua vyumba vya wageni vya mahoteli.

3) Kudumisha Utalii wa kitamduni ikiwemo kuboresha michezo kama riadha, mpira wa miguu, sanaa nk ili kutangaza nchi.

4) Kuunda upya Shirika la ndege la Taifa ili liwe chachu ya kuongeza mapato ya fedha za kigeni nchini.

5) Kutumia Timu ya taifa ya mpira wa miguu *(Taifa Stars)* kutangaza nchi kwa kuwekewa



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 20 8/27/15 3:32 PM

lengo la kufika kombe la dunia kabla ya mwaka 2025 kwa kujenga shule za michezo katika kila mkoa wa Tanzania, Mashirika ya Umma kuwa na timu za michezo na mashindano ya michezo mashuleni kuimarishwa.

6) Kutumia Sanaa kama vile nyimbo na filamu ili ziwe nyenzo za kutangaza nchi, kuongeza ajira kwa vijana kupitia vipaji vyao na kuongeza mapato ya fedha za kigeni.

### 5.2.4 Madini, Mafuta na Gesi Asilia

Sekta za Madini, Mafuta na Gesi Asilia ni sekta za maliasili ya nchi yetu. Sekta hizi zinaweza kuzalisha mapato ya kutosha ya Serikali ili kuboresha sekta nyingine kama vile Kilimo na uwekezaji katika Afya, Elimu na Hifadhi ya Jamii.

Chama cha ACT Wazalendo kitaielekeza serikali kuchochea mabadiliko makubwa katika sekta hizi za uvunaji wa maliasili ya nchi kwa kuchukua hatua zifuatazo:

1) Maliasili zote za madini, mafuta na gesi asilia ziwe mali ya wananchi KIKATIBA na uchimbaji wake lazima uwe na kibali cha wananchi *(free prior informed consent)*.

2) Mfumo wa uchimbaji wa maliasili hizi ubadilike kutoka mfumo wa sasa wa kutoa leseni na kukusanya kodi na mrahaba kwenda mfumo wa umiliki na ukandarasi. Mwekezaji

awe mkandarasi, arejeshe gharama zake na faida iliyobakia kugawana na Serikali kwa makubaliano maalumu. Haki *(mineral rights)* iwe ya Shirika la Umma linalomilikiwa na Serikali na wananchi kwa asilimia 100. Wenye mitaji wawe wakandarasi wa Shirika hilo la Umma kwa mujibu wa mikataba *(Revenue Sharing Agreements)*.

3) Mikataba yote ya uvunaji wa maliasili iwe wazi kwa wananchi. Mapato yatokanayo na mrahaba yagawiwe kwa maeneo yenye shughuli za uchimbaji kwa uwiano maalumu utakaowekwa. Mapato yatokanayo na mali asili ya nchi yawekwe kwenye mfumo maalumu na kutumika kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu, upanuzi wa huduma za afya na elimu, akiba kwa vizazi vijavyo na kuimarisha mfumo wa hifadhi ya jamii nchini.

Sera za ACT Wazalendo zinalenga kuelekeza nguvu kwenye uchumi na kujenga mazingira ya kufanya mageuzi makubwa (transformation) ya kiuchumi, kuwezesha kasi ya ukuaji uchumi kwa zaidi ya wastani wa asilimia 10 kwa muongo mzima na kujenga jamii ya watu walio sawa na huru. Sekta msukumo za uzalishaji ni Kilimo, Viwanda, Usafiri wa kimataifa (transit trade) na Utalii. Sekta msukumo za matumizi/uwekezaji ni Elimu, Afya, miundombonu ya usafiri/ usafirishaji na Hifadhi ya Jamii.



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 22 8/27/15 3:32 PM

Hata hivyo, yote haya hayatakuwa na maana iwapo mfumo wa fedha kupitia mabenki utakuwa umeshikwa na wageni. Nchi yetu haiwezi kuendelea iwapo mabenki makubwa yote yanamilikiwa na watu kutoka nje. Utaifishaji wa Mabenki uliofanyika mwaka 1967 na kuundwa kwa Benki ya Taifa ya Biashara, Benki ya Nyumba na Benki ya Maendeleo Vijijini ilikuwa ni maamuzi ya msingi sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Ubinafsishaji wa Benki ya Taifa ya Biashara na kufilisiwa kwa Benki ya Nyumba ilikuwa ni maamuzi ya hovyo kabisa kupata kutokea katika nchi yetu.

Malengo ya kujenga uchumi shirikishi wenye uhuru mkubwa katika soko la mitaji hayawezi kufikiwa bila ya kuwa na Benki zinazomilikiwa na Watanzania wenyewe. Hivyo, Chama cha ACT Wazalendo kitahimiza kuwa Benki ya Taifa ya Biashara irejeshwe kwenye mikono ya Watanzania kwa kumilikiwa na Serikali 50% na Wananchi na taasisi za wananchi kupitia soko la mitaji nusu iliyobakia. ACT Wazalendo itahimiza pia Benki ya Maendeleo na Benki ya Kilimo kuwa na muundo wa umiliki kama wa Benki ya Taifa ya Biashara.

Mashirika yanayoendesha sekta nyeti katika uchumi kama Umeme, Reli, Bandari, Mkonga wa Taifa, Mafuta na Gesi Asilia, Bima ya Maisha, Benki ya Taifa ya Biashara, Madini ya msingi kama Chuma yataendeshwa moja kwa moja na serikali na kwa ubia na wananchi, na kamwe hayatamilikishwa kumilikishwa kwa wageni.

**Shabaha yetu katika muda wa kati ni kuwa na Pato la Taifa la dola za kimarekani bilioni 90, uwekaji akiba usiopungua asilimia 30 ya Pato la Taifa na makusanyo ya kodi yasiyopungua asilimia 25 ya Pato la Taifa. Tunalenga kuwa Tanzania itakuwa nchi ya 5 kwa ukubwa wa uchumi barani Afrika na ya kwanza katika Afrika Mashariki ifikapo mwaka 2030.**

## 5.3 Afya

Tanzania ni nchi kubwa na yenye idadi kubwa zaidi ya watu katika ukanda wa Afrika Mashariki. Pamoja na kwamba uchumi umekuwa ukikua kwa takribani asilimia saba (7) kwa mwaka, ukuaji huu haujionyeshi katika kuboreka kwa hali ya maisha ya wananchi wa kawaida. Kwa mujibu wa Taarifa ya Sensa ya Idadi ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, kumekuwa na ongezeko la idadi ya watu kufikia asilimia 3 kwa mwaka na idadi ya watu ambao wanaishi katika umaskini wa kutupwa (ufukara) imeongezeka kwa idadi ya zaidi ya watu milioni moja. Ongezeko hili la idadi ya watu maskini linamaanisha ongezeko la watu ambao wanashambulika zaidi na magonjwa yanayozuilika na ambao watahitaji zaidi huduma za afya sasa na katika siku za usoni. Hata hivyo kiasi kidogo cha fedha kimekuwa kikitengwa kwa ajili ya huduma za afya.

Idadi ya vifo vya watoto wachanga na mama waja wazito bado ipo juu na tumeshindwa



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 24 8/27/15 3:32 PM

kufikia malengo ya Millenia. Kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii za mwaka 2013, takribani akina mama 450 kati ya 100,000 wanaojifungua hufa na asilimia 43 tu ya akina mama waja wazito hupokea huduma za Kliniki ya waja wazito, na asilimia 51 pekee ya mama waja wazito hujifungua kwa msaada wa wataalamu wa afya.

Idadi kubwa ya watanzania bado wapo katika hatari ya kuambukizwa au kupata magonjwa yanayozuilika kama vile malaria na UKIMWI. Malaria ndiyo ugonjwa unaoua watanzania wengi zaidi (hasa watoto wachanga) ukifuatiwa na UKIMWI na kifua kikuu, na yote haya ni magonjwa yanayozuilika na kutibika na/au kudhibitika. Kwa mfano, inakadiriwa kuwa watanzania milioni 1.6 wanaishi na VVU/ UKIMWI na kila mwaka zaidi ya watu 100,000 huambukizwa na zaidi ya watu takribani 86,000 hufa kila mwaka kutokana na UKIMWI. Hii imesababisha watoto zaidi ya milioni 1.5 kuwa yatima na kuhitaji hifadhi ya kijamii. Tanzania ni nchi ya 15 kati ya nchi 22 zenye wagonjwa wengi wa kifua kikuu (TB) na hii ndiyo sababu kubwa ya vifo kwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWI.

Idadi ya wananchi wanaougua magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile magonjwa ya moyo, figo, kisukari na kansa imeongezeka. Magonjwa haya yanaweza kuepukika kwa kuwa mfumo wa ugunduzi wa mapema katika ngazi ya msingi.

Tanzania pia ni miongoni mwa nchi katika bara la Afrika zenye idadi ndogo zaidi ya wataalamu wa afya. Kwa mfano, kwa takwimu za mwaka 2010 kuna madaktari 0.4 na wauguzi/wakunga 2.8 kwa kila watu 10,000, ukilinganisha na wastani wa madaktari 2.8 na wahudumu 6.7 kwa nchi zinazoendelea.Ukosefu wa wataalamu wabobezi na vifaa tiba umesababisha wananchi kupelekwa nje kwa ajili ya matibabu na kugharamiwa kwa fedha nyingi.

Sekta ya afya pia inakabiliwa na kuchakaa kwa miundo mbinu na ukosefu wa huduma za msingi kama vile madawa, vifaa tiba, vitendanishi na vitanda katika wodi za wagonjwa. Kutokana na uchakavu wa miundo mbinu na kukosekana kwa huduma za afya katika mahospitali ya umma, wananchi wengi hawaoni kama hospitali ni sehemu salama ya kupata huduma. Matatizo haya kwa kiasi kikubwa yanasababishwa na ukosefu wa raslimali fedha, vitendo vya rushwa, kukosekana kwa ubunifu na uongozi bora katika hospitali za umma.

Takwimu za mashirika ya kimataifa za mwaka 2013 zinaonyesha kuwa ni nusu tu ya watanzania wote ndio wanaopata maji safi na salama, na hali ni mbaya zaidi kwa upande wa vijijini. Watoto 10,000 hufa kila mwaka kutokana na kipindupindu kwa kunywa maji yasiyo salama. Hali hii pia humuongezea mama ugumu wa maisha kwa kuwa anatumia muda mwingi kutoa huduma nyumbani badala ya kufanya kazi za uzalishaji.



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 26 8/27/15 3:32 PM

### 5.3.1 Mpango wa ACT Wazalendo kuhusu Afya

Katika kukabiliana na changamoto za afya zilizoanishwa hapo juu na kuboresha huduma za afya, falsafa itakayoongoza sekta ya afya chini ya Serikali ya ACT Wazalendo ni kuwekeza katika huduma za kinga. **Shabaha yetu ni kila mtanzania awe na bima ya afya ifikapo mwaka 2025**. Serikali itachukua hatua zifuatazo katika kuimarisha sekta ya afya:

i) Kuchukua hatua za dharura katika kuimarisha huduma za mama na mtoto katika vituo vya afya ili kuzuia vifo vya watoto na mama wajawazito, ikiwemo:

   a. Kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa wahudumu wa afya katika vituo vya afya na hospitali zote

   b. Huduma zote za msingi kuhusu afya ya watoto na mama wajawazito zitakuwa bure katika hospitali za umma na binafsi. Katika siku 100 za mwanzo za utawala wa ACT Wazalendo, itaundwa Tume ya Wataalamu katika sekta ya afya na uchumi kuanisha huduma za msingi za afya kwa mama na mtoto ambazo serikali ikizigharamia zitaleta tija katika kumaliza vifo visivyo vya lazima kwa watoto na mama wajawazito.

ii) Kufufua na kuimarisha mfumo huduma za afya ya msingi ikiwemo elimu ya afya kwa



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 27 8/27/15 3:32 PM

jamii ya kitanzania na kuhakikisha huduma za afya zinapatikana kwa usawa na kwa wakati.

iii) Kujikita kwenye afya kinga kwa jamii kwa kutumia mbinu shirikishi na kuibua mipango yenye tija.

iv) Kupitia upya sheria iliyoanzisha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ili kumwezesha na kuhakikisha kuwa kila mwananchi anakuwa na haki ya matibabu na huduma za afya kupitia mfumo wa umma

v) Serikali itatenga bajeti maalumu kwa ajili ya kupanua mafunzo ya kada zote za afya katika vyuo vikuu vya umma na kuweka ushirikiano maalum na vyuo vya binafsi vya afya ili viweze kutoa wataalamu wengi zaidi katika fani za afya. Serikali itaanzisha *'scholarship'* maalumu ya kupeleka watumishi wa afya kwenda kusomea utabibu katika vyuo vya nje kwa maeneo ambayo utaalamu huo haupatikani hapa nchini.

vi) Kupitia upya muundo wa mishahara ya watumishi katika sekta ya afya ili kutoa motisha zaidi kujiunga na kubaki katika sekta hii.

vii) Kupitia na kuimarisha mfumo wa utengenezaji, uagizaji na usambazaji wa dawa na vifaa tiba ili kuhakikisha vinapatikana ubora wa hali ya juu na kwa



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 28 8/27/15 3:32 PM

wakati. Viwanda vya ndani vya madawa vitapata nafuu maalumu ya kikodi.

viii) Bajeti ya Wizara ya Afya itakuwa *'ring fenced'*, ikishapitishwa na Bunge hapatakuwa na mamlaka nyingine yeyote ile itakayoipunguza.

ix) Serikali itaimarisha ushirikiano na sekta binafsi ya afya ili kuongeza huduma za matibabu ambazo awali hazikuwepo nchini.

x) Kuanzisha mpango maalumu wa miaka mitano wa kukarabati miundo mbinu ya hospitali za umma katika ngazi ya Wilaya, Mikoa na Taifa kwa kuwashirikisha wadau wa maendeleo ndani na nje ya nchi.

xi) Kuanzisha mfuko wa maji vijijini *(Rural Water Fund)* utakaotumika kuendeleza na kulinda vyanzo vya maji vijijini na kukarabati miundo mbinu ya maji mijini na katika majiji.

xii) Wananchi watahamasishwa ili waendelee kujielimisha kuhusu umuhimu na namna ya kutunza vyanzo vya maji na mazingira kwa ujumla.



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 29 8/27/15 3:32 PM

## 5.4 Elimu

### 5.4.1 Mtazamo wa ACT Wazalendo

ACT Wazalendo inaamini kwamba elimu ndiyo uti wa mgongo wa maendeleo. Bila kuwekeza kikamifu katika elimu na kuhakikisha kwamba watu wengi iwezekanavyo wanapata fursa za elimu bora, mipango ya maendeleo haiwezi kufanikiwa. Tafiti nyingi zinaonyesha kwamba ili Taifa liweze kupiga hatua ya maana ya kimaendeleo lazima elimu msingi iwe kwa wote kwa kipindi kisichopungua miaka kumi (ikiwemo elimu ya sekondari) na angalau asilimia isiyopungua 20 wawe na kiwango cha elimu ya juu.

Kiwango chetu cha elimu kwa maana ya idadi na ubora bado kinakabiliwa na changamoto nyingi ambazo bila kuzitatua mapema iwezekanavyo mchango wa sekta ya elimu katika maendeleo ya nchi hautaonekana, na kwa kweli hatutaweza kupiga hatua zozote za maana za kimaendeleo. Baadhi ya changamoto na matatizo katika sekta ya elimu ambayo Serikali ya ACT Wazalendo itayashughulikia kwa haraka ni hizi zifuatazo:

a) Kushuka kwa idadi ya watoto wanaojiunga na elimu ya msingi. Takwimu za hivi karibuni zinaonyesha kuwa ni asilimia 78 tu ya watoto wenye umri wa kwenda shule ndiyo walioandikishwa katika shule za msingi. Hii ndiyo kusema zaidi ya asilimia 20 ya watoto wenye umri wa elimu ya msingi hawapo mashuleni



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 30 8/27/15 3:32 PM

b) Zaidi ya asilimia 20 ya watu wazima wenye umri kuanzia miaka 15 hawajawahi kupata elimu yeyote rasmi nchini

c) Asilimia zaidi ya 50 ya watoto wanaomaliza elimu ya msingi hawapati fursa za kujiunga na elimu ya sekondari au ufundi

d) Ni asilimia 2.4 tu ya watanzania ndiyo wenye elimu ya juu kwa ngazi ya shahada ya kwanza. Idadi hii ni ndogo mno na inaifanya nchi yetu kuwa miongoni mwa nchi tatu Afrika na duniani zenye kiwango kidogo cha watu wenye elimu ya juu

e) Uduni wa ubora wa elimu inayotolewa katika ngazi mbalimbali na hasa katika ngazi ya elimu ya msingi na sekondari. Tafiti zinaonyesha kwamba ni watoto watatu tu kati ya watoto kumi waliopo darasa la tatu ndiyo wenye uwezo wa kufanya mahesabu ya ngazi ya Darasa la Pili. Aidha, takribani watoto watatu kati ya kumi waliomaliza darasa la saba hawana maarifa ya kumudu mahesabu ya darasa la pili. Katika miaka ya hivi karibuni ufaulu katika mitihani ya Taifa ya Kidato cha Nne yameshuka sana hadi pale serikali ya CCM ilipoamua kushusha kiwango cha ufaulu ili kuwawezesha wanafunzi wanaofeli kuonekana wamefaulu!

f) Unyonge wa watanzania kumudu lugha ya Kiingereza. Katika ukanda wa Afrika, ni

watanzania pekee ambao hawamudu lugha ya Kiingereza na/au lugha nyingine ya kimataifa. Inakadiriwa kwamba ni asilimia 16 pekee ya watanzania ndiyo wanaoweza kuwasiliana kwa lugha zote mbili yaani Kiswahili na Kiingereza. Hali hii imekuwa ikikwamisha ufundishaji na ujifunzaji kwa kuwa walimu na wanafunzi hawamudi somo la Kiingereza ambalo ndilo linalotumika katika elimu kuanzia elimu ya sekondari hadi elimu ya juu.

g) Kushuka kwa ari ya kujisomea miongoni mwa vijana wa Kitanzania, kutokana na, pamoja na sababu zingine, kutokuwepo vyanzo vya maarifa katika sehemu mbalimbali nchini na hasa vijijini

### 5.4.2 Mpango wa ACT Wazalendo kuhusu elimu

Ili kupanua fursa na kuboresha viwango vya elimu katika ngazi mbalimbali, Serikali ya ACT Wazalendo itachukua hatua zifuatazo:

i) Kuwahimiza wazazi na walezi katika kuhakikisha kwamba wanawapeleka watoto wao kuandikishwa shule, na kuweka utaratibu imara zaidi wa kisheria utakaotoa adhabu kwa wazazi/walezi ambao hawawapeleki watoto wao kuandikishwa shule.

ii) Kufufua mpango wa maktaba za jamii (community libraries) katika kila Jimbo.



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 32 8/27/15 3:32 PM

iii) Ili kupanua wigo wa elimu ya msingi kufikia miaka 9-10 kama ilivyo kwa upande wa Zanzibar, Serikali ya ACT Wazalendo itaanza utekelezaji wa sera mpya ya elimu inayounganisha mfumo wa elimu ya msingi na sekondari ili kufanya elimu ya msingi kuwa miaka 10.

iv) Kwa kuzingatia matokeo ya tafiti yanayoonyesha kuwa walimu ndio kisababisha kikubwa cha mafanikio ya elimu na katika kuwawezesha wanafunzi kujifunza, na kwamba motisha ni muhimu katika kuwachochea walimu kufanya kazi kwa bidii na weledi, Serikali ya ACT Wazalendo itaweka utaratibu maalumu wa kimaslahi utakaovutia na kuwabakisha walimu kubaki katika kazi ya ualimu. Aidha, Serikali ya ACT Wazalendo itaweka mfumo wa motisha kwa walimu utakaokazingatia utendaji na mafanikio katika kuwawezesha wanafunzi kujifunza (performance based incentive system). Aidha, serikali itaweka utaratibu mpya wa usimamizi kwa walimu ili kuhakikisha kwamba wanatekeleza wajbu wao kikamilifu.

v) Ili kupanua wigo wa elimu ya juu mapema iwezekanavyo, Serikali ya ACT Wazalendo itachukua hatua zifuatazo:

   a. Kuanzisha mpango wa muda mrefu wa ujenzi wa vyuo vikuu katika kila kanda.

b. Kuanzisha mfumo nyumbulisho wa usajili katika vyuo vikuu ili kuongeza idadi ya wahitimu wenye sifa za kujiunga na vyuo vikuu.

c. Kuongeza idadi ya shule sekondari ya juu (Advanced secondary schools) ili kupanua wigo wa wanafunzi wenye sifa za kujiunga na elimu ya juu.

d. Kuanzisha utaratibu wa kutoa *scholarship* katika vyuo vikuu vya umma kwa wahitimu wote wenye sifa za kujiunga na vyuo hivyo.

vi) Kufufua na kuimarisha mfumo wa mafunzo ya lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi wote wanaojiunga na Kidato cha Kwanza.

vii) Katika kutafuta suluhu ya muda mrefu katika changamoto zinazoikabili sekta ya elimu, Serikali ya ACT Wazalendo itaunda Tume ya Kitaifa ye Elimu yenye wajumbe wabobezi katika masuala ya elimu kutoka ndani na nje ya nchi ili kutathmini mfumo mzima wa elimu na kutoa mapendekezo mfumo bora zaidi utakaowawezesha watanzania kukabiliana na changamoto za Karne ya 21.

viii) Kufungua vyuo vya ufundi stadi kila Wilaya na katika kila kambi ya JKT. Kufungua vyuo vya ufundi mchundo kila Mkoa.



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 34 8/27/15 3:32 PM

# 6. Mikakati ya Utekelezaji

Ili kutekeleza kikamilifu vipaumbele vilivyoanishwa katika ilani hii, Serikali lazima iwe na vyanzo vya uhakika vya mapato. Lengo la Serikali ya ACT Wazalendo ni kupunguza vya kutosha utegemezi wa misaada na mikopo ya nje. Serikali ya ACT Wazalendo inalenga kujenga uwezo wa ndani ya kukusanya mapato ili kuiwezesha serikali kutekeleza majukumu yake ya kuhudumia wananchi kwa tija na ufanisi wa hali ya juu.

Hivi sasa Serikali inakusanya mapato kwa kiwango kidogo sana kulinganisha Uchumi wa nchi (GDP). Kwa mujibu wa takwimu za uchumi za mwaka 2015, mapato ya serikali ya kikodi ni 11% tu ya Pato la Taifa (GDP). Kwa viwango vya kimataifa, ili serikali ipate rasilimali fedha za kuendesha Serikali ni lazima uwiano wa mapato ya kikodi kwa Pato la Taifa ifikie 25%. Hilo ndio lengo la Serikali itakayoongozwa na ACT Wazalendo. Ili kufikia lengo hili, Serikali ya ACT Wazalendo itachukua hatua zifuatazo:

6.1 Kuongeza shughuli za uzalishaji mali ili kuwezesha wananchi kuwa na kipato. Kodi hutozwa kutokana na mapato ya wananchi na makampuni. Shughuli za uchumi zikipanuliwa watu wengi wanaajiriwa na hivyo Serikali kukusanya Mapato mengi zaidi kutoka kodi ya mapato *(personal income taxes)* na kodi za matumizi *(Consumption taxes)*. Ni wajibu wa Serikali kuweka mazingira bora ya biashara kukua na ajira kuongezeka ili kupata mapato zaidi. Serikali ya ACT Wazalendo itatekeleza kikamilifu hatua mbalimbali za kiuchumi ili kuongeza shughuli za Uzalishaji mali katika



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 35 8/27/15 3:32 PM

sekta vipaumbele kama ilivyoainishwa kwenye sehemu ya 'kujenga uchumi shirikishi wenye kuzalisha ajira nyingi na bora.

6.2 Kuondoa Misamaha ya Kodi isiyo ya lazima na kutunga sheria itakayo hakikisha kuwa misamaha ya kodi haizidi 1% ya Pato la Taifa. Misamaha yote ya kodi itawekwa wazi, itakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na ukaguzi huo utawekwa wazi ili kudhibiti matumizi mabaya ya misamaha ya kodi. Hatua hii peke yake itaongeza uwiano wa Mapato ya Kikodi kwenye Pato la Taifa kwa 2% zaidi.

6.3 Kudhibiti mianya ya ukwepaji kodi hasa katika Idara ya Forodha ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ambapo mwaka 2013/14 peke yake Mapato yaliyopotea kutokana na bidhaa zilizoingizwa nchini bila kulipiwa kodi ilifikia tshs 900 bilioni. Serikali ya ACT Wazalendo itatunga sheria kudhibiti bidhaa zinazosafirishwa nje kupitia bandari zetu *(transit goods)* na kutekeleza kikamilifu mkataba wa Afrika Mashariki kuhusu Forodha ya Pamoja. Hatua hii itaongeza uwiano wa Mapato ya kikodi kwenye Pato la Taifa kwa 1% zaidi.

6.4 Kuweka mfumo mpya wa kodi za kimataifa ili kuzuia makampuni ya kimataifa *(MNCs)* kumomonyoa wigo wa kodi *(Base Erosion and profit shifting)* kwa kushiriki kikamilifu katika kampeni za kimataifa za kurekebisha mfumo wa kodi za kimataifa *(International Tax Justice Network),* kupitia mikataba ya kikodi *(double*



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 36 8/27/15 3:32 PM

*taxation treaties)* na nchi nyingine ili kuzuia ukwepaji kodi na kujengea uwezo kitengo cha kodi za kimataifa *(International Tax Unit)* ili kudhibiti ukwepaji kodi. Tanzania hupoteza mapato zaidi ya 7% ya Pato la Taifa kupitia makampuni makubwa ya uwekezaji. Hatua hii itaongeza uwiano wa Mapato ya kikodi kwenye Pato la Taifa kwa 5% zaidi.

6.5 Kupanua wigo wa kodi kwa kuhakikisha kila raia mwenye kipato analipa kodi kwa kujaza *(tax returns)* kila mwaka.

6.6 Kurahisisha mfumo wa kodi ili kuondoa mizengwe na kuwezesha watu kulipa kodi bila shuruti kwa kushusha kiwango cha chini cha kodi ya wafanyakazi (PAYE) mpaka 9% na kiwango cha juu kabisa kuwiana na kodi ya ongezeko la thamani (VAT). Vile vile kodi ya Mapato ya Makampuni itawianishwa na VAT.

6.7 Maduhuli yote ya Serikali yatakusanywa kielektroniki, hati zote za ardhi zitaunganishwa na namba ya mlipa kodi (TIN) na Mamlaka za Usimamizi na udhibiti (regulatory bodies) hazitakuwa na mamlaka ya kukusanya mapato. Mamlaka ya kukusanya Mapato ya Serikali itakuwa TRA peke yake.

6.8 Kupambana na Ufisadi, Kuimarisha uongozi bora, kupiga vita rushwa na kusafisha uozo ili kudhibiti Mapato na Matumizi ya serikali kwa kuchukua hatua zifuatazo:

(i) Kutekeleza kikamilifu sera ya serikali ya uwazi *(Open Government Policy)*

(ii) Kuweka mazingira ya kisheria ili kuimarisha na kuendeleza uhuru wa vyombo vya habari ili viweze kutoa habari za kweli na kwa wakati kwa wananchi kuhusu utendaji wa serikali

(iii) Kuipa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mamlaka zaidi ya kukamata na kushtaki watu na taasisi wanaotuhumiwa kwa rushwa.

(iv) Kuanzisha Kitengo cha kupambana na rushwa kubwa *(Serious Fraud Office)*.

(v) Kubadili mfumo wa kisheria kwenye masuala ya rushwa na biashara haramu za madawa ya kulevya kwa kugeuza uthibitisho wa mali halali kutoka kwa Jamhuri kwenda kwa mtuhumiwa *(reverse of burden of proof).*

(vi) Kuunda upya Jeshi la Polisi ili kuliimarisha kitaalamu,kiweledi na kulinasua na umateka wa kisiasa ambalo limo katika utawala wa sasa.

(vii) Kupiga marufuku mtu yeyote aliyepatikana hatia ya kula rushwa kufanya kazi na/au biashara katika taasisi ya serikali.

(viii) Kuweka utaratibu wa kisheria utakaohakikisha kwamba makampuni yote yatakayopatikana na hatia ya kutoa au/na kupokea rushwa mali zao zinataifishwa.



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 38 8/27/15 3:32 PM

(ix) Kupunguza ukubwa wa serikali kwa kuwa na wizara zisizozidi 15.

(x) Kuhuisha mchakato wa mabadiliko ya Katiba kuanzia pale iliyokuwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba ilipoishia.

(xi) Kuimarisha mahusiano ya kiutendaji kati ya serikali na taasisi za kiraia. Serikali itaanzisha utaratibu wa kisheria wa kuzipatia ruzuku taasisi za kiraia ili zipunguze utegemezi katika mataifa ya magharibi.

(xii) Kuibadili Taasisi ya Mwalimu Nyerere (Kigamboni) kuwa Chuo cha Mafunzo ya Uongozi. Utawekwa utaratibu wa kisheria kuhakikisha kwamba watu wote wanaochaguliwa au kuteuliwa kwenye nafasi za uongozi wa Umma wamekuwa wamepitia mafunzo ya uongozi.

(xiii) Kuandika upya sheria ya maadili ya Viongozi wa Umma kwa kurejesha Miiko ya Uongozi kama ilivyoainishwa katika Azimio la Tabora.

Kwa hatua hizi Serikali itakayoundwa na Chama Cha Wazalendo (ACT Wazalendo) itakuwa imeweza kufikia makusanyo ya Mapato ya uwiano wa 25% ya Pato la Taifa na hivyo kuweza kuendesha nchi bila ya utegemezi mkubwa wa misaada na mikopo kutoka nje. Uwekaji akiba mkubwa utakaotokana na kuimarishwa kwa Hifadhi ya Jamii nchini utawezesha Serikali kutekeleza miradi mikubwa ya Maendeleo

ya muda mrefu kwa fedha za ndani na hivyo kukwepa kuingia kwenye minyororo ya mikopo kutoka nje. Tutajenga Taifa linalojitegemea.

ACT Wazalendo tunataka kufufua utaifa wa Tanzania ili kila Mtanzania aone kuwa ana wajibu wa kujenga nchi yake kwa ajili ya leo na vizazi vijavyo. Tunataka kufufua uzalendo wa Taifa kwa kurejesha imani ya wananchi kwa viongozi wao kwa kutokomeza ufisadi kupitia Miiko ya Viongozi. Kujenga uchumi shirikishi wenye mfumo madhubuti wa uwajibikaji na unaowezesha kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi afanye kazi na kupata ujira unaotosha ni moja ya njia bora zaidi ya kujenga uzalendo miongoni mwa wananchi na viongozi wa Taifa hili. Tunataka Tanzania ambayo kila raia ana haki sawa ya kupata Elimu bora na Huduma bora za Afya. Tunataka Tanzania ambayo kila raia ana Hifadhi ya Jamii. Tunataka Tanzania yenye usawa.

Chama cha ACT Wazalendo kikichaguliwa Watanzania watakuwa wamechukua hatua ya kwanza kuelekea kuhuisha misingi iliyoimarisha taifa na sera zake zitalenga kufufua uzalendo, upendo, umoja na mshikamano wa Watanzania wote bila kujali rangi, kabila, dini, jinsia na wala ufuasi wa chama cha siasa. Tutakuwa tumeanza hatua ya kufikia ndoto yetu ya Taifa lenye kujitegemea kiuchumi na kiutamaduni, na ambalo linalinda na kudumisha usawa, ustawi wa jamii, uwajibikaji, demokrasia na uongozi bora.



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 40 8/27/15 3:32 PM

# WIMBO WA TAIFA




1. Mungu Ibariki Afrika, Wabariki Viongozi Wake, Hekima, Umoja na Amani, Hizi ni Ngao Zetu. Afrika na Watu Wake.

   Ibariki, Afrika, Ibariki, Afrika,

   Tubariki, Watoto wa Afrika

2. Mungu Ibariki Tanzania, Dumisha Uhuru na Umoja, Wake kwa Waume na Watoto, Mungu, Ibariki, Tanzania na Watu Wake

   Ibariki, Tanzania, Ibariki, Tanzania,

   Tubariki, Watoto wa Tanzania.



ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 41 8/27/15 3:32 PM

ACT-Wazalendo-Ilani 2015.indd 42 8/27/15 3:32 PM